MRADI WA KIMATAIFA WA KIFEMINIA
MAFUNZO LINGANISHI YA NCHI MBALIMBALI YA
HARAKATI YA WANAWAKE NA JINSIA
NA USOMI

NCHI: TANZANIA

Jina la Mhojiwa: Mariam Hamdani

Jina la mhojaji: Anneth Meena

Mahali: Unguja, Zanzibar

Tarehe: 12/15/2022

Chuo Kikuu cha Michigan
Taasisi ya Utafiti wa Wanawake na Jinsia
1136 Lane Hall Ann Arbor, MI 48109-1290
Simu: (734) 764-9537

Barua Pepe: um.gfp@umich.edu
Tovuti: http://www.umich.edu/~glblfem

© Regents of the University of Michigan, 2022

Mariam Mohammed Hamdani alizaliwa Mkunazini, Zanzibar Tanzania Visiwani. Bi. Mariam ni mwandishi wa habari mbobezi na pia na mwanaharakazi. Mwanzilishi wa Bendi ya Taarab ijulikanayo kama Bendi ya Tausi Ochestra.

Bi. Mariam, ametumika kama jaji katika misimu mitatu ya Tuzo za Filam zijulikanazo kama Tuzo za Filamu za Emerson za Zanzibar (2017 - 2019). Vile vile anauzoefu mkubwa katika programu za sanaa na utamaduni. Anatumika katika bodi mbalimbali kama vile Chama cha Hakimiliki cha Zanzibar (COSOZA), Baraza la Habari la Tanzania (2006 - 2008), Jumuiya ya Urithi wa Mji Mkongwe (2009 mpaka sasa). Pia, ni mmoja wa waanzilishi na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maendeleo na Elimu kwa Vijana (ZAYEDESA) (2000 mpaka sasa);Mjumbe wa Bodi/Mdhamini wa Jumuiya ya Urithi wa Mji Mkongwe (2009 - mpaka sasa); Mjumbe wa bodi Wanawake na Maendeleo Kwa Wote (WODFA) kutoka 1990 - 2000; Makamu mwenyekiti wa Baraza la Muziki na Sanaa Zanzibar (2005 - 2010); Makamu Mwenyekiti Tume ya Utangazaji (2005 - 2010).

Bi. Mariam amehitimu kozi mbalimbali hivyo kuwa na Stashahada na vyeti kutoka Taasisi mbalimbali: Stashahada ya Mahusiano ya Kimataifa na Maendeleo kutoka Taasisi ya Mafunzo ya Jamii Hague nchini Uholanzi (1982 - 1983); Stashahada ya Sera ya Mawasiliano na Mipango ya Maendeleo kutoka Taasisi ya Mafunzo ya Jamii Hague nchini Uholanzi kwa ushirikianao na Baraza la Afrika la Mawasiliano na Elimu (1983); Stashada kwenye Uandishi katika maswala ya Afya, Programu hii ilidhaminiwa na wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na wadau wa Maendeleo kutoka Finland, kupitia asasi yao ya FINIDA, Taasisi za Elimu ya Juu ikiwa ni pamoja na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania, na Chuo Kikuu cha Tampere cha Finland (1985 - 1987); Stashahada (Daraja la Kwanza) ya Uandishi wa Habari kutoka Chuo cha Uandishi wa Habari, Dar es Salaam, nchini Tanzania (1979 - 1981); Stashahada ya Historia na Filolojia kutoka Chuo Kikuu cha Frendship Moscow nchini Urusi (1964 to 1965); Cheti katika Mpango wa Kimataifa wa Watangazaji- Msingi wa Kielimu wa Wanawake wa Marekani katika Radio na Televisheni, Inc. (1978, Marekani); Cheti cha Usimamizi wa Huduma za Habari Uongozi kutoka Taasisi ya Mashariki na Kusini mwa Afrika ya Arusha Tanzania (1981); Cheti katika Mwenendo Mpya wa Habari, Mawasiliano na Elimu kwa ajili ya maendeleo ya Jumuiya za Mto Nile Sudan na Misri (1982); na Cheti cha Uzalishaji wa Programu za Redio kutoka Kituo cha Mafunzo cha Sauti ya Ujerumani, Cologne (1985).

Bi. Mariam ameandaa na kuratibu matukio kadhaa likiwemo Tamasha la kwanza la Muziki na Utamaduni Zanzibar mwaka 1994, Mkutano wa Umoja wa Wanawake wa Umoja wa Mataifa kwa Nchi za Afrika kuhusu Amani uliofanyika katika Hoteli ya Bwawani Zanzibar mwaka 1999, na Kongamano la Kimataifa la Muziki na Ngoma za Asili ambazo zimekuwa wa nchi za Mashariki — iliyofanyika Bwawani Hotel Zanzibar mwaka 1996.

Bi. Mariami amekuwa na nyadhifa kadhaa: Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Biashara, Viwanda, na Utalii kuanzia mwaka 2002 hadi 2004; Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Habari (Redio, Televisheni na Magazeti) kuanzia mwaka 2000 hadi 2002; Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Habari Utamaduni Utalii na Vijana 1990 hadi 2000; Naibu Mkurugenzi Sauti ya Tanzania Zanzibar 1989 hadi 1990. Pia amefanya kazi na vyombo vya habari vya kitaifa na kimataifa - Idhaa ya Kiswahili ya Sauti ya Ujerumani

kuanzia 1986 hadi 1988; Idara ya Chumba cha Habari cha Televisheni - mkuu wa waandishi wa habari, msomaji wa habari, na mtayarishaji wa vipindi vya habari kutoka 1978 hadi 1981.

Anneth E. Meena, alizaliwa 1971, ni mtafiti, mwanaharakati na mfeminia. Bi. Meena ni mshauri wa kujitegemea kwenye maeneo mbalilmbali ikiwa ni pamoja na mazingira, Afya na maswala ya Jinsia. Amefanya kazi na mashirika mbalimbali kwenye nafasi mbalilmbli ikiwa ni pamoja na mratibu wa ufuatiliaji na tathmini World Vision, ofisi ya Arusha (2000); Mratibu wa mradi wa Kituo vya Ubora na Ufanisi kupitia shirika lisilo la kiserikali lijulikanalo kama Jukwaa la Wanaelimu Wanawake wa Kiafrika ambapo program hii ilibobea katika kuzingatia jinsia katika mtaala na ufundishaji unaozingatia jinsia (2001 - 2002). Alikuwa mmoja wa waasisi wa shule ya sekondari ya upili iliyojulikana kama Raida akiwa meneja wa kwanza wa shule na baadaye kuwa mkuu wa chuo cha kati wa kwanza (2007 - 2017). Bi. Meena amefanya kazi kama mshauri wa kujitegema katika mashirika mbalimbali ya haki za wanawake yakiwemo TGNP Mtandao; Mfuko wa Wanawake Tanzania; Soma. Vile vile amefanya kazi za tafiti mbalimbli ikiw ni pmaoja na mabadiliko ya tabia nchi na Taasisi za elimu ya Juu ikiwa ni pamoja na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania na Chuo Kikuu cha Michigan, Marekani.

Ms. Meena ni mwanachama wa mitandao mbalimbali kama vile mtandao wa kupinga rushwa ya ngono, mtandoa wa haki ya uzazi, ujinsi na afya.

Bi. Meena ametunukiwa tuzo mbalimbali za kitaaluma ikiwa ni pamoja na Tuzo ya Hammad kwa kutambua kazi ya kipekee yenye mada ya kimataifa iliyotolewa na shule ya Huduma za Umma ya Wagner, Chuo kikuu cha New York Marekani. Vile vile ni miongoni mwa wanawake wawili wa Africa waliopata udhamini wa masomo kutoka kwa Oprah Winfrey na kusoma katika Chuo Kikuu cha New York, Marekani katika kipindi cha 2004 - 2005. Pia amepokea udhamini wa Ford Foundation na kupata nafasi ya utafiti katika kituo cha Kimataifa cha Utafiti wa Wanawake, Washington, DC, Marekani mwaka 1999. Amepokea tuzo ndogo ya utafiti kutoka Baraza la Maendeleo ya Utafiti wa Sayansi ya Jamii.

Ms. Meena ana shahada ya kwanza katika sayansi ya Mazingira na Jiografia kutoka Chuo Kikuu cha Cape Town, Cape Town, Afrika ya Kusini (1996). Shahada ya Uzamili ya sayansi ya watu (Demografia) kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania (2000); na Shahada ya Sayansi katika Usimamizi wa Huduma za Umma kutoka chuo Kikuu cha New York, New York, Marekani (2005).

Anneth Meena: Hello, sikusikii. Hello unanisikia? Karibu.

Mariam Hamdani: Asant asante nakusikia sasa.

AM: Unanisikia sasa?

MH:Nakusikia vizuri.

AM: Asante na pole kwa changamoto hiyo.

MH: Ah! Si unajua huku na mitandao yetu nayo inamatatizo nimejaribu kufungua mpaka kwenye laptop lakini naona hivo hivo lakini sasa hivi naona afadhali.

AM: Asante sana. Naomba uweke camera yako nikuone vizuri.

MH: Okay! Sasa unaniona?

AM: Ndio nakuona asante. Kwanza tuanze maana naona umekuwa na siku ya nzito leo. Pole sana na hongera.

MH: Asante Sana asante.

AM: Kwanza nikushukuru kwa kutenga muda wako na kukubali kushiriki katika utafiti huu ambao ni utafiti wa wanawake na jinsia mradi wa kimataifa wa kifemenia uliothaminiwa na chuo cha Michigan. Lengo ni kukusanya taarifa za kihistoria na kuzihifadhi mazungumzo ya wanawake ambapo uanaharakati wao umechangia kwenye mapambano ya kiwanaharakati na mambo muhimu ya wanawake. Kwa hiyo siku ya leo tutatumia takribani lisaa limoja kuzungumzia maeneo Matano: Maisha yako kwa ujumla na kazi, tafakari yako ya kazi, maoni yako kuhusu mahusiano kati ya femenia na harakati na inavyohusiana na kazi yako, mtazamo wako na maoni yako kwenye mtazamo mzima wa takwa la wanawake, na mwisho Mahusiano yako kama yapo, kati ya kazi unazozifanya na hizo za wanaharakati wengine nchini.

Kwahiyo tukianza kabsa labda tuzungumzie kuhusu historia ya maisha yako. Unapofikiria kuhusu ulipo leo unaonaje safari yako ilipokufikisha leo, nini ambacho unaona unaweza kusimama na kujivunia, nini unaweza jivunia kama mafanikio yako makubwa katika kazi yako. Karibu.

MH: Asante sana. Nadhani umeshajua mimi nimezaliwa hapa Zanzibar nimekulia Zanzibar alafu baadae ndio nimetoka nje kusoma na nimerudi. Lakini sasa naweza sema kwamba malezi yetu ya zamani kidogo yamechangia sana kuwajenga hasa wanawake. Japo kuwa ilikuwa inaonekana kama watu wa ndani lakini ilisaidia kwasababu kila mara unaambiwa uwe na hadhari na nashukuru kwamba mimi nimekuwa mwandishi wa habari wa miaka mingi. Mtangazaji, nimetangaza mpaka sauti ya Ujerumani tulishirikiana miaka miwili. Na wakati wote nilikuwa najitahidi sana kuwasaidia hasa wanawake, wengine walikuwa wanashawishi nilikuwa nakwenda foreign pale mara nyingine napata fomu za kujaza.

Wanawake kuwasaidia nasaidia mi nilikuwa tu naona nafanya kawaida kumbe nilikuwa nafanya kitu cha maana. Sasa nilipokuja kuwa mkurugezi ni redio hapa Zanzibar, sauti ya Tanzania Zanzibar wakati ule ndio hata Dr. Salim Mnari alipokuja kuzindua jengo jipya alisema wazi, inaonekana wanawake hapa wamesoma zaidi kuliko wanaume. Kwa sababu mimi niliwaita nikawaambia sikilizeni siku zote tunapiga kelele wanawake tunaonewa wanawake tunazalilishwa. Sasa hivi mmeshapata fursa sasa ndio muitumie, kwa hivyo kuna wengine waliokuwa form two mimi nikazungumza na cousin wangu akawa anakuja kuwasomesha. Wakafanya mtihani wa form four tukafanya kila mbinu wakaingia Tanzania School of Journalism (TSJ) kwahiyo walifaulu wengine. Kuona wawili watatu wamefaulu na wale wengine wakapata moyo wakaendelea. Halafu mimi vile vile niko katika sport/michezo, nakumbuka niliwasaidia sana wanawake wakawa wanapata fursa na kwenda majumbani kwao kuwaombea ruhusa. Kwa sababu wengine walikuwa hawaruhusiwi mpaka aende Bi Miriam, mpaka niende mie hapa jamani. Hawa watu nakwenda nao Dar es Salaam, nakwenda nao Zambia sijui tunakwenda Egypt tunakwenda wao walikuwa wakisafiri wakipata fursa wakicheza mi nilikuwa katibu wao Zanzibar kwa miaka 12. Kwa hivyo kwa upande ule nilikuwa nasaidia sana hasa wanawake nilikuwa nashangaa kwamba families kumbe zilikuwa zikiniamini sana, ilikuwa hawaruhusiwi kabsa kama mimi sijaenda kuwachukua. Halafu,baadae nilipofanya kazi redio ndio hivyo nikaonekana kwamba ni hodari nasaidia ndio nikawa mkurugenzi. Baadae nikawa naibu katibu mkuu wizara ya habari utamaduni utalii na vijana. Pia, nilikuwa nadeal na mambo ya habari lakini wakati huo huo nikawa nadeal na mambo ya Sanaa. Unajua katika kazi mara nyingine kunakuwa na uonevu wa hali ya juu hasa hawa wanaume. Wanakuwa wanakufikiria kwamba kwanini wewe unajiona unajua unafanyaje yaan matakwa yao hayakubaliki kwahiyo wanaweza wakakublock. Na katika maisha nashukuru mimi mama yetu alivyotulea na marehemu kaka yetu. Yeye alikuwa anasema mkazane katika maisha, mambo ya kuonewa msikubali, usiwe mgovi, usiwe mshari lakini msikubali kuonewa hadi mtu anakuonea kupindukia. Sasa nakumbuka nilipokuwa wizara ya habari, nilipokwenda kule ilionekana yule waziri na katibu mkuu walikuwa hawanitaki kabsa. Kwa hivyo walikuwa hawanipi kazi nimekwenda kuripoti kwa rais hawa bwana hawanipi kazi huu ni mwezi wa tatu sasa hawanipi kazi kabsa. Lakini kwa sababu mimi nilipata course moja pale ESAMI ya uongozi kwa hiyo nilipata secretary mzuri nilimwambia niletee mafile nikasoma ile wizara yote nikajua juu chini chini juu. Sasa baadae ikawa naripoti mpaka kwa rais still huletewi file hata moja la kazi na mimi nilikubalika nashughulika na mambo ya habari kwa hiyo hapo hapo mimi nikageuza kwa sababu mimi mwenyewe nilikuwa napenda utamaduni nilikuwa na kikundi cha utamaduni kwa hiyo nikaona kwanini nisiimarishe upande huu. Nikaimarisha sijui kama mnamkumbuka marehemu Bi Kidude, marehemu Bi Kidude ilikuwa juhudi yangu kumchukua Ujerumani. Kwasababu nilipokwenda Sauti ya Ujerumani nilikutana na jamaa Bern Salim akataka kuja kurekodi hapa nyimbo za taarab kwa kikundi kimoja cha mstafa. Mimi nikamwambia ni bora urekodi vikundi mbalimbali, kuna vikundi vya wanawake kuna vikundi vya wanaume kwa hiyo sio kikundi kimoja na kwa bahati walikuja kurekodi kikundi sahilia karekodi Roel. Sasa baada ya mwaka mmoja wa mauzo wakasema sisi tutakualika nje Ulaya tukaalikwa. Sasa katika orodha ile niliwekwa na Bi Kidude loo! Ikawa issue, yule Rukia katolewa akatiwa mwanamke mwingine tukaona huyu katolewa kawekwa mtu mwingine sasa ikabidi na Bi Kidude asiende kwa hivyo nikaitwa na marehemu Dr. Omari nilikuwa nasikilizana nae sana. Kwa sababu mimi wakati ule nilipokuwa mtangazaji nilimhighlight sana katika vipindi vyake yeye alikuwa daktari wa

wanyama hajawa bado makamu. Kwahiyo tukawa bado tuna uhusiano mzuri. Sasa akaniita akaniambia, “tumezungumza mengi nikawa najua kuna jambo anataka kuniambia”. Akaniambia mbona naskia umetoka ujerumani kuja kumchukua Bi kidude na mbona watu wanasema anatumia neno wild nikamwambia sasa mbona Bi kidude anatumia Wild sisi tunamwita Wild. Oh! Mbona, “nikamwambia no Bi Kidude ni mtu wa masihara ukimtukana na yeye ni mtu wa masihara atakutukana hivyo hivyo. Akasema kwa hiyo hadi kuabishana nikamwambia hapana hawezi kutuabisha mimi nakuhakikishia huyu ndie atayetupa sifa kwa sababu mimi nilipokwenda nje Ujerumani. Holand kusoma pale international relation nilikuwa napenda hizi festivals matamasha yaan ikitokea tu mimi nipo kama siku hiyo sina masomo basi nashinda huko huko unajua wale unawezashinda eneo lile lile kila kitu kiko huko. Kuna vyoo, vyakula unaweza ukashinda kutwa huko. Sasa nikamwambia mimi mbona nimeona wazee wanavyoheshimiwa kwenye haya matamasha? Na pahala popote unalitafuat lile soko kwamba huyu ataweza. Ah! Basi kama utaona sawa basi, si unamjua tena Dr. Omari marehemu maskini. Basi ndio wakamuona Bi kidude Ujerumani basi yule Bern nakumbuka akawa ananiambia “Mariam I never thought Bi Kidude such a star” nikamwambia huyu ndio maana mimi nimemleta kwa sababu mimi nilijua huyu atawashinda wengi. Na alipokwenda ndio hiyo changamoto hizo, wale wasanii wakamwambia hapana yale mambo ya kutia yaleli hapana unajua maana ya yaleli? Ni ile aaaaaah aaaah wazungu hawataki. Akaja kuniambia Bi Mariam wamenikataza nikamwambia we tulia. Wakati ukiimba we nitazame nitakupa ishara wakati wa kutia hiyo yaleli. Kwa sababu mimi nilijua pale kuna Wajerumani wengi wanaasili ya Uarabuni. Kwahiyo mambo kama yale ya yaleli nini aah! Yaan pale nikampa ishara akapiga yaleli bwana wangu bwana wee!. Bwana kulikuwa na fujo sio ndogo wengi wakisema yalehi yehali ewalaa. Basi tena kuanzia hapo magazeti yote yakamuandika sana basi kuanzia hapo akawa tu anachukuliwa, tulienda nae Ufaransa tukaombwa tuende nae Japan ingawa sasa hivi anawekwa wekwa kila kikundi ndio mwisho yake yeye akapata tuzo nyingi akaendelea mpaka alipofariki. Na mimi nikaanzisha kikundi changu cha wanawake kinaitwa Tausi ambacho kikundi hiki Tausi kimepata mualiko nchi nyingi Holand tumekwisha kwenda, mwezi wa pili tulikuwa Ujerumani na kabla ya hapo tumekwenda Uturuki tumekwenda Egypt hata umoja wa nchi za Africa. Walikuwa na mkutano mwaka ule wa 2010 walitualika ndio mara ya kwanza alikuja mbibi mmoja akatuona sisi akasema mimi nitakualikeni akatualika. Kumbe watu wanapenda hivi vikundi vya wanawake sasa sisi vikundi vyetu vya wanawake vinapiga nyimbo za kama taarab asilia za mapenzi, lakini tunaimba vilevile nyimbo za kupinga uzalilishaji. Tunapinga uzalilishaji kwa watoto na wanawake, nyingine tunaingia kwenye kampeni hizi za mambo ya afya hasa zile za kuchanjisha watoto. Watoto wengi wanakuwa wanaachwa hawapelekwi hospitalini halafu macho yao yanapovuka unakuta hawaoni. Kwahiyo tumeshaimba nyimbo kama hiyo mambo ya kansa na nyingine kwa hiyo sasa tunafikiria tulenge nini ila saa zingine radio zinatuuzi hawazipigi saa zingine ila tukipata fursa kwenye tamasha tukipata fursa kwenye shughuli tunaziimba hatuziachi. Watu ah! Bi Mariam hamuogopi? hapana kama wao hawazipigi sisi ndio tunaimba sasa ilikja festival tulizipiga mbona watu walitusifia mmefanya vizuri bwana. Umenifahamu, sasa katika maisha bila shaka kulikuwa na changamoto nyingi tena sisi wa familia za kizamani huna ruhusa hiki huna ruhusa vile mimi nilitamani ningepiga music zamani ila sikuweza kuomba alafu huthubutu kusema kutokana na mila zetu. Lakini sasa napiga chombo kile kinaitwa kanunyi unajua, sema mimi sijapenda kuimba napenda tu kuwaimarisha wasanii zaidi. Lakini pia nasema kwamba nilipokuwa chombo cha habari mpaka leo hii ni

mwanachama wa TAMWA na nashukuru wananiheshimu sana na nimeshakuwa katia board katika vipindi vya miaka kati. Sasa hivi nimekuwa kama mshauri tu na ikitokea kitu hasa hapa Zanzibar vijana wanataka kwenda pahala mm! Bi Mariam tunakuomba bwana sisi wasanii wako tupeleke nawaambia najua mimi twendeni. Maana hata mimi katika maisha yangu nilisaidiwa hasa nilipokuwa kwa radio. Radio wakati ule mi kijana we nifikirie mimi mika 20-30 nyuma nilikuwa vipi, nilikuwa mrembo alafu uvaaji wangu haukuwa na mtandio wala nini navaa jeans, viatu vya kisigino sasa wanaume wanavyokukupapatikia utakwenda kufanya interview gani wewe wanaume wakubwa wenyewe waliokuwepo hapa basi maskini alikuwepo jamaa mmoja anaitwa Joseph Asama amefariki sasa hivi marehemu. Yeye alikuwa mkuu wa vipindi basi nilikuwa nasikilizana nae na mwenyewe alinipenda maana tukitaniana. Njoo unisaidie bwana maana nataka interview fulani lakini sasa kumuendea yule ah! Yule? Hupati interview pale wewe utafanyiwa vituko. Ananipeleka anafuatana na mimi hahah lakini na yeye alikuwa na mikasa alikuwa anakaa pale pale mimi nafanya interview namaliza. Sasa akirudi baadae anawahadithia jamani mmm nilimuweza mheshimiwa yule maanake yake alikuwa anamtumbulia macho anammezea mate Mariam lakini hawezi mwambia kitu Mariam nilipo basi. Lakini kanisaidia sana na kila siku namuombea dua maana yake nilipata vipindi vingi nilionekana hodari nafanya vipindi vya maajabu. Ndio nikapata apointment yangu ya kuwa mkurugenzi wa redio pale ikasemekana hodari maana yake wengine hawawezi wanaogopa. Ukifika kule huyu atakutaka hujamtaka inakuwa balaa unakuja nyumbani usiku utafanyiwa balaa. Lakini sasa mimi nikipata mheshimiwa yeyote anayenitaka namwambia boss yupo namuombea dua kila siku walahi maana yake yeye alikuwa mojawapo kati ya wale walionisaidia nikapanda juu. Alafu pia kulikuwa na mzee Sheikh Salim mzee alifariki alikuwa na umri wa miaka mia lakini ilikuwa kila siku Bi Mariam stahimili hawa watu. Walahi anakuja mtu anapelekewa mwandishi anaandika juzi nzuri zinatoka. Siku ya pili anakuja yule yule mheshimiwa nyuzi gani hii mnanipa wanakuja waandishi wa habari wazuri hamnipi kwani yule mwanamke yuko wapi. Nikamwambia Salim tena sikiliza we stahimili hawa watu bwana hawana lolote lakini maadam we unajua nenda kaandike pakukimbilia ni wewe. Sasa hizo ndio changamoto nilizopata na nikikumbuka huwa nacheka. Basi safari moja aliniita waziri alikuja pale reli akanikuta pale “haa sijajua mimi wizara yangu ina wanawake wazuri hivi”, mimi nikanyamaza kimya haya kesho nitaitwa na kweli nikaitwa nikaenda akaniambia haya mimi sijakuitia lolote isipokuwa leo saa kumi uje hapa nataka nikuchukue tukatembee mimi wapi? “Kwani wewe mtoto mdogo si umeshanifahamu? “ Nikamwambia sijakupata unakusudia nini nieleweshe. “Nakusudia nakutaka mimi” Nikamwambia sikutaki. “Akaniambia unathubutu kuniambia mimi sikutaki naweza chukua mkasi nikukate” Nikamwambia nikate na huo mkasi nikambamiza mlango na kuondoka pale pale.

Niliporudi redio bahati nzuri nilikuta mkutano alikuwepo mheshimiwa marehemu Kamishina nafikiri walikuwepo wanajeshi na police na walinzi wa ile Institution pamoja yupo mkurugenzi etc. Hapo hapo nikaomba kuingia ndani nikaomba nikawahadithia imetokea hivi na hivi ala! Wanawazimu hao wanafikiria wewe. Alafu baadae nikaja kusikia kumbe yeye ndio kawaida yake wale wafanyakazi wake wako vile vile. Ilikuwepo siku moja jioni alitokea mlinzi wake nasikia alifungua mlango kamlaza mtu juu ya meza, wewe mheshimiwa gani wewe alaa!. Nilipowaambia pale nikaambia we tulia wala usiwe na wasiwasi hawezi kukufanya chochote naam. Siku ya pili nasikia matangazo kapelekwa

mkuu wa mkoa huko kusini sijui wapi mwingine katolewa uwaziri hahah. Nikasema kweli nimebahatika na kumbe mara nyingine ukiwa unajiheshimu na hata wale watu wakajua ni kweli huyu anajiheshimu hata uwe vipi mzuri vipi watakuheshimu na watakuonea huruma. Basi hizo ndio mambo ambayo siwezi kuyasahau lakini hata niipokuwa chuo cha waandishi wa habari kulikuwa na mwalimu mmoja baadae akawa ananitania nilishamaliza chuo basi anasema sasa hivi wewe si umeshamaliza chuo si unaweza nikubalia eti nikamwambia kwa pale nilikukataa kwa sababu gani? Basi alikuwa ananipa marks ndogo mpaka kuna jamaa mmoja alikuwa ananiambia walahi mimi ningekuwa wewe walahi ningetafuta pesa nikatafuta watu wamtoe macho. Mtu atakuaje unaandika paper nzuri hivi anakupa 40 huyu? Basi lakini namshukuru nikawa na nguvu nikamfuata mkuu wa chuo nikamfahamisha nikamwambia but why? Mimi nasoma najitahidi ila hebu angalia hi paper yangu hii. Akatazama akaniambia basi katulie wala usiseme kuwa wewe umekuja hapa. Yaan usisikie bwana wanaume wengine ni wakorofi na ukiwa mwanamke na hasa kama mimi nilikuwa, sijisifu ila nilikuwa mzuri sio hivi niko na miaka karibia 80 tena both hahah. Watu bado upo na competition na wazee, kwa hiyo basi malengo yangu mimi hasa nilitamani nifike zaidi lakini ndio sikufanikiwa unajua mtu unafanya kwa mfano, nilisoma Holland pale international Relations postgraduate nikaja nikasoma tena nikasoma international communication nikaja tena nikaapply mambo ya wanawake lakini wakaniambia ingalikuwa haya mambo yanahusiana na habari wangenikubali kwahiyo mimi nikasema basi mimi nitaenda sauti ya Ujerumani miaka miwili. Walitaka nafikiri kuniongezea muda kutokana na masuala yao lakini mimi siwezi baridi mara naumwa na kifua mimi nikataka kurudi nyumbani nafurahia zaidi. Pesa nazitaka lakini pesa za kuumwa kila siku za kazi gani hata nilipokwenda Marekani bahati mbaya siku zile, unajua hapa Zanzibar kulikuwa kama mtu una asili ya kiarabu au kingazija ulikuwa huwezi kusafiri. Sasa kulikuwa na nafasi ya kwenda Marekani kwa miezi sita au mitatu kwa study tour basi kulikuwa na rafiki yangu wa kihindi bahati nzuri mume wake akawa yule Thabiti Kombo nikaja siku moja nikamwambia kuna safari hii lakini ngumu akasema utarudi? Maana wengi wakitoka wametoka hawarudi nikamwambia mimi nitarudi akasema una uhakika nikamwambia mimi nakuhakikishia mimi siwezi kumuacha mamangu hapa mtu mzima anateseka kwa sababu ya mimi kukaa Marekani. Basi yule bwana alikuwa na nguvu katika serikali na Bi Kombo nilipokataliwa pale alisema aah mtoto wetu huyu atakwenda tu na kurudi. Basi nimeenda Marekani nimekuta nafasi imetangazwa ya wanawake siku zile Mwahamina amekwenda Ujerumani wamekwishakunishikilia nikasema hapana. Maadam nimemuahidi yule mzee afu kama sijarudi nitewaharibia watu wote nikikaa hapa Marekani. Nikarudi ni changamoto hiyo, siku moja baraka akaniuliza nimekuuliza ilikuaje umepata fursa kubwa kama zile alafu umeacha nikamwambia hapana. Mimi roho yangu iko nyumbani mimi roho yangu iko na wazee wangu hawa ndio walionilea sasa mamangu mzee nimuache pekee yake hapa ndugu zangu wako bara maana yake Menji alikuwa Moshi siku zile ndio baada ya kuonana na Menji huko chuo kikubwa tukaonana na wao walisomea uchumi wakapelekwa Moshi. Swaliha yeye alikuwa yuko UN katika haya mambo ya world food program haya alikuwepo ni mimi na Bi Rabiha lakini mamangu alikuwa attached na mimi zaidi nikasema hapana siwezi kumuacha mamangu. Hizo ni mambo ya dunia lakini sijutii nafurahi kwamba niko na furaha hapa nilipo sina kitu kikubwa lakini niko na furaha nadhani vile vile ukiamua sio tu unaamua kwenda Ulaya unamuacha mtu aliyekulea wakati wote ndio ukamtupa. Nafikiri ukiamua hivyo hata mungu anakupa baraka, ninavyoamini

mimi na ndio maana niko hapa nimeshakua mimi makamu wa rais wa baraza la habari la Tanzania. Baraza la habari we unalijua ni kubwa.

AM: Nalijua.

MH: Mimi nilikuwa vice president pale katika kipindi kile cha pili alafu sio tu vice president walinipa fursa nikafanya utafiti wa kitabu nikaandika juu ya Zanzibar media Zanzibar ilikuwa thirteen centuries alikizindua rais. Alafu baadae katika mashindano walinipa tuzo award, walinipa award nilipata award kwamba ni mfanyakazi bora excellence in journalism na hata mwalimu wangu aliniambia wewe bwana hawajakupendelea bali wewe umeandika hicho kitabu. Hichi kitadumu katika miyoyo ya watu ingawa kile kitabu walikitoa bure sasa hivi ndio nafanya mpango ili iweze kuwekwa mitandaoni ili watu wakisome bure hata mimi nilijitolea hata pesa nilizopata hazikuwa nyingi lakini nikasema wacha nikiandike. Kwahiyo nashukuru katika maisha yangu nimekutana na maprofessor wakubwa kina Shifudi nimekutana na bwana Omani nimekutana na watu kina marehemu Othman na wengine pia nimejifunza kwao mambo mengi. Na hapa vile vile nashukuru wanawake nimeshirikiana nao hasa miaka ya mwanzo miaka ya zamani nilipokuwa kijana nimeshirikiana nao sana Afushirati nimeshirikiana nao sana nilikuwa kwenye zile kamati za wanawake. Lakini pia baadae nilipokuwa mwandishi wa habari na mara kwa mara nasafiri mara kusoma hizo short course nyingine ndefu, nikaona tena siwezi shiriki. Lakini mpaka hivi leo ikiwa jambo lolote mimi nawaambia mi niiteni tu. Niko tayari maana hata katika kampeni za siasa tunazungumzia siasa kuwaambia watu wasigombane, msipigane. Sijui niseme mengi maana we umeniuliza mengi lakini sijui sasa kwa njia hii hauathiri kitu?

AM: Unasema?

MH: Kuna msikiti hapa sasa hivi itapiga kelele ngoja niangalie WIFI yangu niweze kusogea hapa. Lakini hapa sasa unanisikia?

AM: Ndio nakusikia.

MH: Hebu nikumbushe nizungumzie nini kingine.

AM: Okay! Cha pili umeyagusia historia ya maisha ya kazi yako umeeleza sehemu mbalimbali ambazo umefanya kazi. Lakini labda ambacho ningependa kujua ni nini kilikuhamazisha katika kazi unayoifanya?

MH: Mimi kusema kweli mwanzo nilikuwa nataka kusomea udaktari. Udaktari wa akili lakini mwanzo tulisafiri tukiwa wadogo mimi nilikuwa mdogo wakati ule wa siasa, siasa za hibu siasa za sherazi. Tukaenda China.

AM: Samahani naomba uweke camera yako vizuri, imekaa juu naona juu zaidi.

MH: Sawa nafanya hivyo. Sasa wakaniambia itabidi uchukue miaka kumi iiiiii kumi na mimi ni mdogo namimi nalia maana nilitaka kurudi nyumbani. Unajua saa zingine usitoe mtoto mdogo kwenda kusoma nje, kwa sasa hivi ni tofauti sasa watu wameshazoea kukaa

mahostel. Sisi tumelelewa kizamani shule nyumbani hutoki kama hawa watoto wetu siku hizi wanakwenda maparty wanakuwa wana mitazamo tofauti. Sisi basi siiti ushamba ila unakuwa nyumbani tu sasa unamtoa mtoto nje unamwambia akakae miaka 10 mimi nikawaambia mimi sitaki. Sasa kakangu alipokuwa Urusi nikakimbilia Urusi kule. Kwa hiyo nikiwa huko ndipo niliposomea Historia na Physiology kule nilifuarahia kidogo yeye alikuwepo na ilikuwa ikitokea kitu kidogo yeye ananichukua kwenye madancer nikawa kidogo mstaarabu. Basi baada ndio nikageuza sasa na kurudi hapa Zanzibar history imetolewa na literature yote kwa sababu literature ilikuwa mkisoma mnasoma ya Uingereza inaongelea mambo ya nje sasa hivi tunataka literature ya watu wetu wenyewe hapa hapa. Na vile vile hata lugha tunataka iwe yetu.

[Interrupted]

Basi mimi nilifanya kazi shirika la habari la Urusi ni shirika la habari la Urusi nikapata kidogo changamoto nikaona hapa Zanzibar siasa zilizokuwepo na baadae nikaja kuolewa na…ndio hivyo nilikuwa naonekanaonekana mzee Moyo wakati ule alikuwa waziri wa Elimu akaniona akaja kwetu kutoa pozo ile narudi kazini naambiwa kaja hapa mzee Moyo na mzee Kaojere nilitetemeka maana huyu mzee Kaojere alisifiwa kwenda msikiti kubwa ya wahindi kule na kwenda kupiga risasi kule nikasema khaa kweli. Sasa mamangu akaniambia sasa huyu inaonekana mtu mzuri nikajua pengine ameogopa lakini mie tena nikakubalia kuolewa nae. Nikakaa nikazaa mtoto mmoja alifariki nikaja kuzaa wa pili sasa baadae wazee wake wakaja kumwambia hapana huyu kila siku anabadilisha maguo unampenda unamnunulia tu magauni kwa hiyo wale wake zako wengine wawili warejee. Maana alimuacha mwingine anaitwa Hadija na mwingine anaitwa Salma mimi ripoti zote anayenihadithia ni yule bibi yake yule mzee maana ni mzee sana yeye hajui cha kuficha yeye anazungumza tu kiwe kibaya kiwe kizuri. Kwahiyo mimi nikawa nashukuru kwa kuwa napata taarifa “akawa anasema nikamwambia lakini kakataa” nikajua hapa kuna matayarisho. Nikakaa sasa siku hiyo ndio akaniambia oh! mamangu babangu, nikamwambia mimi nimetoka kwetu family tofauti na family waliotoka wale wengine. Mimi nimetoka mjini niko center pale nyumba yetu ya mama yetu ghorofa mbili wakati kabla ya mapinduzi alafu hatukuwa matajiri lakini tulikuwa watu wa kati na kati alafu nimefanya kazi taasisi kubwa na kununua nguo nazozitaka. Halafu mimi nimekwenda kule na maguo tele basi akaniambia mamangu kasema ni lazima niwalete wale wanawake wengine maana yake ni nyumba kubwa. Basi nikaanza kuhamishahamisha nguo zangu kidogokidogo maana yake kila mtu alikuwa na kabati lake yeye alikuwa na kabati lake na mimi langu wala hajui kama natoa nguo au vipi. Sasa ile siku ilipofika yeye mwenyewe aliwaleta wake zake kuja pale nikamwambia kaa mwenyewe na zizi lako la ng’ombe mimi siwezi kukaa katika zizi la ng’ombe kabsaa. Mimi wewe nilishajua hawa miaka miwili uliwarejea sijakuuliza kwa sababu kila mtu na maisha yake. Lakini sasa hivi unaniletea mimi hapa huwezi kunilazimisha mie huyo nikaondoka nikaenda kwetu. Baadae akaja kunisikitikia oh! unajua najuta maana niliambiwa na Thabiti Kombo usimlinganishe huyu na wake zako, huyu ni tofauti usifanye hivyo huyu katoka katika ukoo tofauti usimlinganishe. Nikamwambia mimi sirudi maadamu umefanya mambo ya kipumbavu kabsa kuonyesha kuwa wanawake si lolote si chochote unaweza tu kupachika mijitu ndani ya nyumba wakawa watu watatu kila mtu na chumba chake kakae mwenyewe huko na zizi lako la ng’ombe. Basi mimi tena nikaenda redio nilikwenda Ikulu kumuona mzee Karume. Akaniuliza hutaki kurejea kwa

mzee Moyo nikamwambia sitaki akaniuliza sasa unataka kufanya nini nikamwambia nataka kufanya kazi radio maana mimi nilifanya kazi communication agency na niliacha kwa sababu ya kisiasa haikuwezekana mimi kuendelea ndio mwanzo nikaanza kwenda radio. Nikaenda redio nikafurahia redio tunapishana hivi anatuma watu me hata sishughuliki mimi ni mtu mmoja ambapo mtu anapoona anapesa basi afanye anavyotaka na mimi nafanya maisha yangu navyoona sawa. Basi tena ndio tumeendelea nikafanya kazi pale redio baada nikaenda chuo cha uandishi pale Dar es Salaam nikatoka Esami, Esami ni short course lakini ilinisaidia nikasema oh! pale Esami wale wanaosoma Esami kwa kweli wako smart sana. Ile course ya miezi sijui miwili na nusu mmmm ngumu lakini ni lifetime maana mpaka leo hii nikienda kwenye uongozi ningesema mimi ningelikaa pale mwaka mmoja uongozi sijui ningekuwa vipi, hivi kile chuo bado kipo?

AM: Ndio, kipo nadhani kipo.

MH: Basi ndio kilichonisaidia mimi kusoma watu kufanya hivi na kuingia sehemu tofauti na wale wengine wanaoingia uongozi tu. Hizi courses zinasaidia sana japo fupi fupi ila zinasaidia japo watu hawaelewi tu lakini muhimu sana, sababu baadae nilipokwenda Ujerumani nikachukua short course vile vile za uongozi kwa hiyo nikavichanganya. Lakini hii aisee ya Esami ndio iliyonisuka hasa, basi ndio tena nimeendelea kuwepo hapa mara nikipata fursa nasafiri narudi mpaka hivi sasa nimestaafu. Lakini nimestaafu and I'm still happy kwa sababu baada ya kustaafu nilisema hapana why not acha nianzishe kikundi kwa sababu kulikuwa na vikundi vya wanawake hapa Zanzibar vingi tu kulikuwepo Zari bulahi, kulikuwepo Royal Navy, kulikuwa na Banati, Hairia, kulikuwa na Nuru royal, na vyote vikipendwa na vilikuwa na members wengi sana. Tatizo lao lilikuwa wanapokwenda kuimba kwenye harusi wanapigiwa muziki na wanaume, hivyo wanaimba lakini wanaume ndio wanaopiga vinanda vyote na Violin. Sasa yamekujakuja haya mambo ya utalii haya wakawa wanaitwa mahotelini, hotels zinawalipa ataacha mtu pesa zinazolipwa hotelini ukapige vyombo kwa wanawake? Wakapotea mojamoja vikundi vingi vikajikuta hawana wapiga vyombo. Of Course walikuwa na matatizo yao wenyewe maana yake wanawake hawakosi matatizo unajua. Lakini moja ya sababu kubwa ni vyombo navyo hakuna pia kwahiyo vikundi vyote vikafa more than twenty hakuna kikundi hata kimoja. Na mimi nikasema why napenda apige lakini sitaki aingie kwenye group la wanawake na wanaume, mwingine anasema mimi nina mwali wangu hawa wasiolewa sitaki waingie kwenye group la wanawake na ndoa. Nikaanza mimi sasa baada ya kustaafu kununua vyombo second hand hivi violin etc hata jamaa walianza kunong'onezana siku hizi Bi Mariam hazimtoshi ananunu hizi vyombo vyote vya nini haya vitu tele vya nini vyote? Walahi mmoja alizungumza siku zile acha watu waskie watu walicheka. Walahi me sidhani ka Bi Mariam yuko sawa amenunua violins, ngoma sijui nini. Nimehangaika na kuhangaika nimekwenda huko na huku kwenda kutafuta wanawake waje wajifundishe music kila unapoenda wanakutumbulia macho tu. Basi nikaenda pahala moja wakanitumbulia macho nikasema ah! Basi nikarudi nyumbani nikasema basi nimepata hasara pesa sote baada ya kustaafu badala nikae nijinunulie kitu cha maana nimenunua vyombo hivi hapa, Siku ya pili yake napigiwa kengele naambiwa kuna wageni wako hapa wanawake ishirini na tano wamekuja. Haya tunataka kujifunza hivi vyombo basi wakaangalia huku wakaangalia huyu anataka kujifunza violin huyu anataka kujifunza hiki mwingine kile ndio tukaanza. Tukaanza na bahati nzuri alikuwepo Mohamed Elias huyu mwimbaji maarufu hapa Zanzibar wa Taarab

na yeye ni hodari ya kupiga vinanda vyote hapa Zanzibar. Yeye akaahidi nikiweza tu nitawafundisha wote lakini utakachojaliwa utanilipa au usinilipe chochote. Six months sisi tumepanda busara kupiga kuna mtoto alikuwa na bibidii tumepiga wewe nakumbuka marehemu Maimuna aliniambia labda miaka saba watapiga lakini ila miezi sita hawapigi hawa. Asubihi nawaambia njooni saa tatu ila saa mbili wameshafika ikifika saa sita nawaambia nendeni kwenu sasa hawataki we tugaie pesa tukanunue chips hapo wanakula wanakaa mpaka saa kumi. Basi wanaanza kupiga watu wakawamezea mate wakaanza kuwaoa, kuwaoa tu wakaanza kuwazuia wasije. Hebu image tu umeweka effort, na utamshitaki nani nchi hii? Uende mahakamani ukawashitaki oh huyu hapa nimemfundisha na hapa katia saini kwamba nikishamfundisha atatumikia kikundi hiki kwa miaka mitano nani atakusikiliza watakucheka watu. Maana kwa mila zetu sisi na tamaduni zetu basi nakwambia wamewachukua walianza na mmoja wa gitar alikuwa hodari huyo akaja wa violin na wawili wa kanuni kwa mpigo. Wakishakaa kwenye stage wanawaona wazuri hivyo lakini tukabahati kuna wengine wakasema hapana mimi nimemuoa acha aendelee lakini kikundi cha wanawake hatutaki vikundi vingine. Yuko mmoja mpaka kazaa mtoto. Tulialikwa Bagamoyo kulikuwa na festival akasema mme ruksa lakini mtoto asiniachie mimi, hapana. Sasa kikundi chetu sasa kikawa nursery huyu analea huyu ananyonyesha huyu anachemsha maji hahah mpaka tukaenda Bagamoyo tukafanye festival tukafanya vizuri tukarudi. Tuko na mmoja sasa yuko na watoto watatu ila mume wake kampa ruksa nakwenda nae hadi Burundi nakwenda nae Egypt yupo mwingine sasa alipoolewa tu akaambiwa mazoezi tu akulipe elfu tano alafu ukifika stage elfu hamsini. Sisi hatuna hizo hela kumlipa mtu elfu tano mazoezi elfu hamsini stage week moja sijui shilling ngapi basi tukamsamehe. Kakaa nje miaka mitatu sasa hivi karudi yeye mwenyewe kasema niliwaambieni narudi lakini sasa mgeni na huyo mume na siwezi kugombana nae kwa mila zetu sasa hivi wamefahamiana anakuja. Anakuja vizuri na ajabu kumbe alikuwa na kipaji kwa sababu hajapiga miaka mitatu anakuja hapa anashindana na hawa waliopiga juzi juzi ana kipaji. Mwingine alikuja babake hapa analia “mimi naona uchungu Bi Mariam mwanangu anavyopiga vyombo kaolewa mumewe kamkataza sasa mimi siwezi kuingilia kati basi mimi nitamfungulia duka”, kasikitika. Lakini ndio mila zetu, hizo ndio changamoto zinazotukabili lakini mimi bado sivunjiki moyo hawa walioolewa lakini waume zao wanawaruhusu tutaendelea nao sasa hivi tumebaki kumi na katika hao wawili wameshakuwa watu wazima hawahudhurii lakini hawa wengine wanawaruhusu na mara nyingine wanakuja kuwachukua lakini na mimi kitu kimoja ninachokifanya kwa uhakika tukienda tukio kama shamba mfano tukirudi nawapeleka mwenyewe mpaka mlango nagonga mlango au wao wenyewe unawaambia waume zao wanawangoja njiani. Hiyo ndio tabu ya wanawake lakini inaendlea si haba wengine wanafurahi. Nacheka kuna wengine hawataki waingie mwanaume hata mmoja kila kitu mwanamke mpiga picha mwanamke kila kitu mwanamke afu unashangaa hawa watu vipi mbona wale wanaume ndio wanawaandikia vya kule. Mbona sisi tunapenda kujiboost kwa jambo ambalo hatuliwezi lakini sasa huwezi kukataza maana wenyewe ndio wameamua. Mpaka fundi maana sisi tulikuwa tunaazima redio yule fundi anawaandikia sijui namba hii namba moja namba mbili ili ikitokea tatizo watengeneze maana yeye hawezi kuingia ndani wanawake watupu hawataki mwanaume alafu unakujaje mwandikie mwanaume. Sasa siku wakituambia hakuna ruhusa wanawake watupu na we ndo fundi mzuri basi tunamwambia akae pale tunamtafutia kiti kizuri akae pembeni kule. Namwambia akae pembeni huko hata wasikuone unakaa kwa nyuma yetu ikitokea chochote wanawake wenyewe watupu

wameshaamua hivyo. Tuna vipaji vingi tu majumbani tu lakini ndio hivyo serikali haisapoti haiungi mkono kabsa kabsa. Hasa hapa kwa sababu sisi tulipoanza walahi huwezi amini tulikuwa hatuna mpiga ngoma tunao wapiga ngoma wawili lakini hawawezi. Sasa tukiwa na tukio inabidi tumfiche mwanaume apige ngoma basi tulikwenda bwawani walahi nakwambia tumepiga taarab siku ya pili naitwa kwa marehemu Shamhuni. Nikajiuliza kuna nini tena, naambiwa jana alikuwepo balozi wa Misri alikuwa kwenye lile tukio ambalo alilokuwepo mheshimiwa Shamhuni kasema lazima kikundi hiki cha wanawake kiende Gairo ili wale wa kule waone wanawake walivyo wawaone. Sasa najiuliza vipi Gairo na mpigaji ngoma wanaume? Maana yake tulimficha nyuma sasa baada ya watu kuona kuna safari ya Gairo watu wakaanza kuja kushinda hapa kushinda hadi jioni mpaka wakaweza kupiga ngoma. Bahati mbaya ili tunataka kwenda ikatokea tatizo kuna kifaa kilivunjika hatukwenda tena lakini baada ya mwaka wakatualika tukaenda Gairo tukapiga wakatuomba tukaimbe kule Sandrea mko tayari? Tukawaambia tusiwe tayari na sisi twataka pesa! Basi ikawa kila show wanatulipa. Kwahiyo kuna changamoto za wanawake wakishakuakua tu hivi na kuwa wazuri na kuolewa basi huwapati. Sasa wanakuja hapa juzi walikuja watano sasa nikisema niwafundishe hawa kidogo kama moyo wangu unarudi nyuma maana yake ukiwafundisha siku mbili haya wanaolewa unakuwa unawapoteza maana sisi hapa hawalipi wanajifunza bure alafu saa zingine kama mtu hana nauli tunamgaia nauli na akija hapa tunahakikisha kuna maji ya moto kwaajili ya chai, chai ipo, sukari ipo na kahawa ipo na saa zingine wanasema Bi Mariam nimetoka nyumbani maisha magumu nigaie pesa nikanunue andazi nampa ndicho nachoongea. Lakini sasa hivi kinachotia uchungu ni kwamba juzi walikuja wakataka tuende Nisemee pale si kuna chuo hapana sitini elfu sisi hatuna. Lakini sasa mimi nitakufundisheni nipoteze nguvu zangu alafu hao wakiolewa waume zao wanawazuia kidogo inatia uchungu sana. Sijui swala gani tena unataka kuniuliza kwasababu ukiniongoza vile ndio inasaidia.

AM: Nataka kujua mahusiano yako katika harakati je nini mtazamo wako wa harakati kwa ujumla katika kazi zako? Naona umeamua kuwachukua wanawake kuwafundisha kazi ambazo ama tasnia ambazo zilikuwa zinabebwa na wanaume.

MH: Sawa. Na hao wanawake wanakuwa waimbaji. Mimi niko TAMWA na nashukuru kuwa nimeanza nikiwa kijana hadi sasa nazeeka. Kwa hivyo wanavyofanya TAMWA na mimi niko pamoja nao/nyuma yao. Na vile vile kama sasa kama itatokea kitu wanataka ushauri mimi wa kwanza kuingia na kwenye kikundi chetu sisi tumejitolea kwamba tutapambana kwa njia ya nyimbo. Tunapambana kwa nia ya mashairi, tutapiga mashairi kuwalaani wazalilishaji wanaofuata watoto mashuleni kuwabaka na kuwatia mimba za utotoni vitu kama hivyo tunawalaani kabsa. Tunataka sasa hivi kuendelea kwa kupambana tuko tayari kushirikiana vikundi vingine kama sasa hivi magazeti zimejaa stori za watoto wanaoibiwa, watoto wanageuzwa watumwa. Ndio sasa hivi tunataka kutoa nyimbo za kusahihisha hasa wazee. Kwa sababu mimi saa zingine wanachangia kwa upande mwingine hawa watoto kuibiwa kwa mfano kama sisi zamani of course maisha yetu yalikuwa tofauti maisha yetu yalikuwa kutwa kwa ndani na mkicheza nje mnacheza hapo nje ya nyumba na wazee wanawaaangalia wakikuita jina Mariam unaitikia abee. Yaan wote mnaonekana sasa hivi sehemu zote za wazi wamepewa watu wamejenga majumba. Sasa watoto watacheza wapi hivi sasa wanacheza manyumbani na sio manyumbani tu hivi sasa kuna hizo simu hizo watu hawana time na watoto. Na sijui niseme maisha yamebadilika kwa sababu zamani

watu wakiolewa ni miaka 13-14 hadi afikishe miaka 28 ana mjukuu hadi 60 ana vitukuu. Maisha yalikuwa tofauti lakini sasa hivi mama yuko kazini na bibi pengine bado 60 yuko kazini mtoto analelewa na mfanyakazi wa nyumba na mfanyakazi huyo nae ana tabia zake alizotoka nazo kwao. Kwahiyo pengine hata hamuulizi mtoto fanya uhuni sawa chukua simu sawa fanya hivi. Kwahiyo inakuwa kidogo maisha ya watoto wa siku hizi tunaweza kusema wanapendwa maana watoto wananunuliwa masimu makubwa. Wananunuliwa toys kama sisi kipindi kile toys ilikuwa sikukuu mpaka sikukuu unakusanya unajua pesa yangu nitanunua toys leo. Sasa hivi kila siku watoto wananunuliwa nguo zipya kila siku ukipita manyumba utaona nguo zimejaa tele. Zamani tukijifunza hata kushona zile toys za vitambaa unajaza pamba ndani unajifunza huyu toy wangu au watoto wa kiume wanachukua yale nanihi mabua wanatengeneza magari ubunifu nzuri unaona kigari hiki kinakwenda. Tunacheza pia, vishada tunarusha tulikuwa tuna ubunifu na akili zikifanya kazi. Sasa hivi sasa juzi tu kuna mjukuu wangu mmoja nimemrushia kitu kikaanguka, nikamshangaa inamana hapo umeshindwa kudaka? Nikamuuliza kwani shuleni hamchezi netball? Akasema hawachezi netball sasa najiuliza mtoto atakanzana vipi wakati sisi tumecheza netball, volleyball, skirtball etc alafu kulikuwa na lessons zile za kingereza walimu wetu walikuwa wakitupeleka kujifunza English kwa vitendo kwhiyo ilikuwa inamchangamsha mtoto. Halafu Jumatano shuleni hiyo nimezungumzia sana mimi katika redio na television sisi darasa la tano pale Forodhani nilipoenda shule kulikuwa na jenga moja pale sasa hivi limekuwa Morocco kule tulikuwa tunasoma domestic science sasa hiyo domestic science unafundishwa kushona mbali unaanza mpaka unashona ya maua sasa zile za kuweka kwenye maforonya alafu unafundishwa namna ya kuvuma sweta za watoto, socks na vikofia. Alafu vile vile tulikuwa tunafundishwa korosheti na mwisho tukafundishwa sharahani na mtoto kulea. Yaan mimi mtoto wa mwanzo kumkama na kumuosha ni sanamu kubwa hilo sijawahi ona sana kubwa vile unamuosha kichwa maji unahakikisha unatia ya baridi usitie ya moto kwa sababu utamuunguza mtoto hiyo sisahau tangu mdogo. I never forgot. Halafu, baadae tukafundishwa kila aina ya vyakula unavyovijua wewe vya Zanzibar hapa. Mara lipopo, na vingi tu na viungo vyao ukimaliza sasa maana sisi tulikuwa na marehemu Belal tulifundishwa vyakula vya kizungu sasa. Mara christmas cake, fruit cake etc etc kila aina ya vyakula unavyovijua wewe ila siku hizi sasa hamna watoto wanaishia kwenda kununua sijui mnaviita vibanzi. Masufuria machafu haya yamejaa mafuta wanapikia chips ndio wanawanunulia watoto sasa haya ni matatizo maana watoto wanaishia kutumia simu kutwa watoto akili zao yanakuwa ya yaliyomo ndani ya simu. Kwa mfano mimi ukiniambia namna unaitumia simu unajifunza vingi mule ndani maana yake vitu ni vingi. Ubahatike watoto wawe wanaangalia Diamond wawe wanamuangalia Alikiba ushukuru mungu wameenda kwenye music. Lakini wanakwenda kutafuta uhusika na ndio maana tunaambiwa siku hizi watoto wa siku hizi wabaya katika shule. Shuleni utakuta sijui takribani darasa nzima watoto wanaharibiana wenyewe kwa wenyewe mbali ya huharibiwa na walimu sasa watoto wataharibiana wenyewe kwa wenyewe vipi? Wakiulizwa kuna mtu alifanya utafiti akaambiwa aha wanaona kwenye mitandao sasa na wao wataka kujaribu. Sasa nani atakataa wakati hata wazazi hawana muda na watoto hawana wakirudi wanasema wamechoka sasa mimi najiuliza kwani mama zetu walikuwa hawachoki? Kwa sababu sisi tulikuwa tunakwenda shule mama zetu wanakuna nazi wakipika, wakichambua mchele tunakuja nyumbani wale wadogo saa sita chakula tayari. Wakubwa ndio wanarudi saa saba lakini siku hizi hamna wakirudi wanajitupa. Na sisi jioni zamani kulikuwa hamna TV hamna chochote lakini tulikuwa na mabibi wanaotufundisha hadithi, wanatufundisha

kusoma, wanatufundisha mana ukirudi tu unaambiwa upumzike baadae mnacheza hapo nje kuna taa mnaonekana mkirudi tu unaambiwa fanyeni homework mkimaliza homework haya kunyweni chai mapema tu maana yake wazee wetu zamani hawakutaka kila mara watoto waamke usiku kwena chooni wla kufanyaje. Baadae mnaanza kuulizwa haya we umesoma nini? Mimi nimesoma hisopo, nimesoma sungura, sungura na panya. Haya soma asome atododoze hapo haya yule mwingine atasoma methali, methali kumbe kule ndio tunasomeshwa tuna tunakumbushwa yale ya shule, Haya wewe umesoma nini, mimi nimekisoma kitabu cha kingereza haya kisome hicho. Naamini bibi yetu alikuwa hajui chochote lakini anatupa moyo tu kwa kupiga makofi. Na anazisoma hizo hadithi alkini za kiswahili zilizopo zina maarifa sana halafu pia zile hadithi za kufahisha zile za lela tukimaliza michezo sasa kinyurinyurika haya mnacheza pale. Mnaiga tena nyoka huyo, huyu anakwenda huko mwingine huko, huyo kashafika huyo mnajifunza ile kunyanyuka haraka wa mwisho anazomewa kaliwa na nyoka analia huyo basi ilmradi tu. Basi baadae tukishamaliza haya muda wa hadithi sasa, hadithi hadithi njoo basi mtaonywa mkawe na heshima hizo hadithi hazimaliziki hivyo kila siku hadi tunalala. Lakini sasa umuhimu wa zile story baada ya kumaliza ndio mnaambiwa mnajua maana ya hizo stori? Wema hauozi mara hiki ili tu kuwatishia mkae mbali na wanaume maana tulikuwa tunaambiwa mwanaume akikuguzaguza mamako atakufa yaan mnatishiwa ili mkae mbali na wanaume. Lakini sasa hivi utamwambia nini mtu ana simu yake kubwa imejaa mapichapicha na wala mamake hamuulizi hii simu umepata wapi sasa ni tofauti unajua mimi nafikiria kwa sababu mimi na yule jamaa ambae amestaafu tulipanga tufanye film unajua nimeshandika stori mbili kazikubali sana kasema kazipenda. Lakini sasa tatizo nataka kuwaita wale wengine wanaofanya stories lakini wao wanataka tufanye milion mia moja ndio tuandike stori ya kizamani. Pia zamani kulikuwa na uzalilishaji kwa njia zake yakifichika sasa hizo mimi ndio nafikiria niwaite tufikirie kama tunaweza kupata kwa gharama ndogo kama milioni tano au kumi tunaweza kufanya kama zili mbili zote zinazungumzia uzalilishaji lakini very interesting kwamba zinaonyesha utamaduni wa hapa watoto wanacheza kiutamaduni na heshima za wazee wao. Sasa wawili watatu wale wazee waiokuwa wanawakosea wale watoto wanaweza kupata hasara kwa yule mtoto na zikifanikiwa hizi films utaona nimepiga hatua lakini nafikiri nitafanikiwa. Kwa sababu ni zungumza na jamaa mmoja akaniambia sasa sikiliza haihitaji milioni mia bwana, milioni mia films hizo za kina nani zinazopelekwa mbali lakini films za humuhumu tu tunaweza kwenda nazo hata milioni tano sita tukijitahidi pia ni moja kutaka kusaidia uzalilishaji. Kusaidia wanawake mateso ya wanawake na hivi, mimi nitakuwa naendelea kutumia nyimbo nitakuwa natumia hizi film ndogondogo na nimekusudia hilo na nafikiri nitafanikiwa inshallah.

AM: Asante.

MH: Kwa sababu inatia uchungu kuona wazazi, zamani wazazi unajua aah! Wakiita huko chini Mariam naam abee utaitikia uko mbio lakini sasa hivi mwanao hujui yuko wapi aah! Hapa walahi nakwambia imagine TV, anaonyeshwa mtoto TV saa nne ya usiku jamani mtoto huyu kapotea hajulikani wazazi wake aah! Saa nne usiku inamaana mama yake yuko wapi? Na si mara moja si mara mbili. Saa nne usiku mtoto kapotea kaokotwa, how? Inamaana wazazi wengine hawajali na unajitetea unafanya kazi kwani unafanya kazi hadi saa nne za usiku? Na majumbani hawa wanawake hawa, mimi ndio nimefikiria nizungumze na TAMWA tufanye discussion hizi ili hawa wanawake nao wajione maana kila siku wanalaumiwa

wanaume tu. Oh! Wanaume wanawaharibu watoto sasa si ndio mnawaachia majumbani kutwa? Hao wafanyakazi mnaowaajiri utawasikia wengine hawaangalii wewe umeshaona wengine wanajifanya wanawake kumbe ni wanume. Si uanze kumpeleka kwanza police wamjue kama huyu ni mwanamke au mwanaumehatufanyi kuna hadhari sisi wenyewe hatuzichukui, zamani wazazi wanazichukua. Zamani mimi nakumbuka kuna safari moja marehemu mjomba wangu alikuja na alikuwa anaishi Dar Es Salaam basi sijui mambo ya kitoto unajua sijui kitu gani nikaenda kumnong'oneza nikacheka na yeye akacheka. Basi kakaa kaa alipoondoka wee wakaniuliza ulitumwa na nani wewe kwanini ulienda kumnong'oneza usiokuwa na adabu mhuni mkubwa wee hivi wee hivi. Toka siku hiyo nilikoma lakini sasa hivi baba atamchukua mtoto wa miaka kumi na mbili kumi na nne atakwenda nae Dar Es Salaam atakwenda nae hotelini we unaona sawa anapendwa iko wapi respect, wanaume wenyewe hawa kwahiyo kuna mambo ni lazima tuongelee. Hili mimi nitazungumza na TAMWA na wengine hao hebu tufanye hizi discussion kila siku sasa tusiwaachie hao wanawake wanaoona kama ni kulaumiwa alaumiwe wanaume tu kila siku. We unajua hapa ukisikiliza Mawio walahi unaweza tokwa machozi walahi mtoto wa miaka sita anabakwa. How atapatikanaje fursa kama wewe mwenyewe upo yaan haisemeki kabsa utasikia wazazi maisha, maisha gani hayo kwani hujipangii wewe maisha? Jipangie saizi. Kuna wengine mimi nina wajukuu zangu mama yao kama hajapata mtu wa kukaa nao anawaleta hapa na wananiogopa. Siku hizi watu hawaaminiki mtu anaweza gonga mlango akasema mimi mjomba mimi shangazi wako wakaingia watu wawili wakawabaka wakishamaliza watajiondokea. Sasa wazazi nao wamama na wababa na hizi talaka zisizokuwa hazina mpango na hizi vle vile tumezizungumza katika nyimbo. Talaka za hovyo hovyo kuna nyimbo tumeimba kila siku watu wanaachana yaana watoto kila siku wanatupwa tu wababa wanaoa tu kuoa kwao ni kama mchezo hivi. Ni kama karatasi umeikamata na rangirangi unaikamata unaitupia basi, watoto wanateseka hawadumumiwi ukienda mahakamani wewe mahakama ya kazi hiyo ukasikia hizo kesi utakereka yaan kweli zile mila za zamani zimetoweka zamani tulikuwa tunawalaumu wanaume wanapelekwa jangoni wanawake wanapelekwa somo, lakini simu ni somo sasa, simu zimekuwa zimezitawala na kama hatutafanya juhudi kuondoa hii tabia ya watoto kuwa na simu alafu wachezee watakavyo hapana watoto tusiwalalamikie. Maana yake sasa hivi asilimia kubwa ya watoto wameharibika kabsa kabsa na ni kutokana na simu. Tuendelee.

AM: Nilitaka nikuulize ingawaje umezungumzia kidogo. Mwingiliano wa kazi zako pamoja na takwa la wanawake nchini pamoja na kimataifa. Umesema ambapo bado unaendelea kutumika na TAMWA na watu mbalimbali katika kutengeneza film, na hizo organization umekuwa unazifanya nazo kazi sasa ni zipi bado unafanya nazo kazi nje ya nchi na nyingine unazofanya nazo hapa.

MH: Nje ya nchi kwa sasa hivi sina isipokuwa kuna wale ambao wao wanatualika kwa mfano kule Berligin kuna jamaa mmoja ambaye yeye aliwahi kuwa hapa yeye help aid internationally anaitwa Ron Graham. Yeye anatusaidia kwa sababu ya hizi nyimbo sasa nyimbo ztu sisi tunazozifanya ndio hizo za kupinga uzalilishaji ili tuweze kuziendeleza. Lakini kusema sasa shirika la nje ninalofanya nalo kazi hapana sina. Na nikipata fursa hiyo pengine kama nitakuwa na nguvu au sina nitawaandikisha wengine ambao wanauwezo waweze kusimamia lakini zaidi nipo hapo hapo TAMWA na kushirikiana na mashirika mengine kama mikutano za FELA tunazichangia na zaidi na concentrate na hizi shughuli

zangu za rais kwanza mimi nimeshakuwa mtu mzima saizi kumove kama zamani si rahisi hivyo.

AM: Sawa. Nilitaka kuuliza kwa kumalizia muunganiko wa kimataifa na aina za harakati unazozifanya je unamahusiano na wanaharakati wengine au wanataaluma wengine au asasi katika nchi zingine na hayo mahusiano yalijengwaje?

MH: Kusema ukweli huko nje sina, kwa hapa tulikuwa na kama moja mwisho lakini nilitoka mimi mwenyewe kwa sababu ile ilikuwa na wanaharakati wengi sana ambao walikuwa wanapinga uzalilishaji. Tukawa tunakwenda tunapinga uzalilishaji lakini mwisho tukawakwenda tunakutana hatufanyi chochote tunasikia tu hadithi hii hadithi hii. Mimi nikaacha ndio maana nikabaki huku tu TAMWA nikabaki huku kwingine na natamani itokee hiyo ya nje yeyote ambayo kama nitaweza shirikisha nitashirikisha lakini za nje kabsa ziko niko pamoja na kina Fatuma Mallu niko na kina Dr. Sadam, napenda sana tunakutana mikutano mbalimbali yanayohusu uzalilishaji. Lakini iko hivyo hivyo tu na kama mchango wangu natoa tu kwenye kuzungumza au katika radio na television ni kiwango hicho.

AM: Okay! Nakushukuru sana mama Mariam kwa muda wako nashukuru pia kwa majadiliano tuliokuwa nayo naona kwa leo nimekamilisha lakini nikuombe ukipata muda unitumie CV yako pamoja na picha picha ya passport size ili niweze kuambatanisha.

MH: Sawa nitakutumia. Kwahiyo ukisikia kuna pahala mimi naweza kusaidia intenationally unijulishe usiache pia.

AM: Sawa kabsa hakuna neno. Nimefurahi sana kukutana na wewe na nimekusikia sana kwa leo kwa Fatuma Mallu.

MH: Fatuma Hallu ni mpenzi wetu na hodari sana Fatuma hodari sana.

AM: Tukija Zanzibar tutakutembelea.

MH: Sawa njoo kwangu sio pakubwa lakini ukija feel at home.

AM: Asante sana na uwe na mchana mwema.

MH: Samahani hii zoom imetuhangaisha sana

AM: Asante lakini mwisho wa siku imetokea

MH: Ndio tumefanikiwa na mimi nimefurahi.

AM: Sawa asante sana.